

JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS –TAMISEMI

SHULE YA SEKONDARI YA MUKA

S.L.P 213

KASULU

10.12.2020

KUMB.Na.ED/MKSS/JIF/VOL.01/18

ME/KE.....

S.L.P

KASULU

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MUKA

KWA KIDATO CHA KWANZA 2021

1.0.Utangulizi.

Ninayofuraha kukuarifu kuwa umechaguliwa kujunga na kidato cha kwanza katika Shule ya sekondari ya kutwa ya Muka mwakani **2021**.Shule ya Sekondari Muka ipo umbali wa km **10** kaskazini kutoka Halmashauri ya Mji wa Kasulu ulipo..Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe **11.01.2021**,Hivyo unapaswa kuripoti tarehe hiyo na mwisho wa kuripoti ni tarehe...../...../2021.

2.0. Mambo muhimu ya kuzingatia.

2.1.Sare za Shule(Madarasani)

- **WAVULANA;** Kwa wavulana ni suruali (2) za damu ya Mzee (darkred) ziwe za heshima na ziwe na linda mbili ambazo chini hazibani.

-**WASICHANA;**Sketi rangi ya damu ya mzee (darkred) zenye malinda isipokuwa mbele na nyuma panakuwepo linda moja kubwa.Nnguo ziwe za heshima na urefu wa skert ufikie soksi na zisibane.Kwa waoslamu rangi ya Hijab iwe nyeupe kama rangi ya shati.

-**WOTE;** Kwa wanafunzi wote wasichana kwa wavulana wanapaswa kuwa na Shati nyeupe mbili zenye mikono mifupi. Vitambaa vya Suruari na Sketi ni lazima viwe vile vizito vya Suti.

2.2. Sare za Michezo

- WAVULANA; T/shirt ya kijani na Suruali nyeusi pia kila mwanafunzi atatakiwa awe na Trucksuti ya bluu.
- WASICHANA; T/shirt ya kijani na sketi ya kijani Pia kila mwanafunzi atatakiwa kuwa na Trucksuti ya bluu
“Ni marufuku kuchanganya Sare za shule(zile za madarasani) na zile za Michezo.”

2.3. Vifaa vya Darasani.

- Madaftari makubwa 11
- Kalamu za kutosha
- Mkebe wa hisabati (mathematical set 1).

3.0.Sheria na kanuni muhimu za Shule ya Sekondari Muka.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sharia ya Elimu **Na.25** ya mwaka **1978** na kama ilivyoelekebishwa na sharia **Na.10** ya mwaka **1995**. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu ofisi ya Rais –Tamisemi,yenye dhamana ya Elimu chini ya Ofisi ya Waziri mkuu –Tamisemi yenye jukumu la usimamizi na Uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shulenii.

- a) Heshima kwa viongozi,wazazi,wafanyakazi wote wanafunzi wengine pamoja na jamii kwa ujumla ya Muka Sekondari Muka.
- b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shulenii nzima.
- c) Kushiriki kwa umakini kufanya maandalio ya jioni (**preparation**)
- d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nydingine utakazopewa.
- e) Kufahamu mipaka ya Shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
- f) Kutunza uafi wa mwili, mazvazi na mazingira ya shule.
- g) Kuvala Sare za Shule wakati wa wote unatakiwa.
- h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
- i) Kutunza Mali za Umma.

3.1.Makosa yafuatyo yanaweza kusababisha mwanafunzi kufukuzwa au kusimamishwa masomo;

- i) Wizi
- ii) Uasherati na ushoga
- iii) ubakaji
- iv) ulevi na matumizi ya madawa ya kulevyta kama vile Kuvuta bangi,cocaine,mirungi,kubeli n.k

- v) kupigana na kupiga
- vi) kuharibu kwa makusudi mali ya umma
- vii) kudharau bendera ya Taifa
- viii) kuwa mjamzito au kupata miba/kusababishia mimba
- ix) kuoa au kuolewa
- x) kutoa mimba
- xi) kugoma,kuchochea au kushiriki kuvuruga Amani na usalama w ashule au watu.
- xii) kukataa adhabu kwa makusudi.
- xiii) kuwa na simu ya mkononi.


- 3.2 Mambo mengine muhimu yanayopashwa kukamirishw na kuwasilishwa shulen na mwanafunzi siku ya kuripoti ni pamoja na;**
- a) Medical Examination Form,ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali.**Fomu hii ni muhimu ikabidhiwe kwa mkuu wa shule siku ya kuripoti shulen.**
 - b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki migomo,fujo na makosa ya jinai.
 - c) Fomu ya mwanafunzi na mzazi kukiri kukubaliana na sharia,kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

4.0.Hitimisho.

Tafadhali soma kwa umakini maelezo/maagizo hayo na kuyatekeleza kikamilifu.Aidha,enfdapo mwanafunzi hatafika shulen mapema kwa sababu yoyote ile mzazi/mlezi amtaarifu mapema mkuu wa shule kabla ya tarehe **11.01 2021**.Kwa wale watakaokwenda shule za binafsi au za mashirika ya Dini nao pia watoe taarifa.

“KARIBUNI SANA SHULE YA SEKONDARI MUKA”

Nawatachia maandalizi mema;



JANUARY G. DANIFORD.

MKUU WA SHULE

**MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI MUKA
S. L. P 213
KASULU**